



SWAHILI

Bw. Dijon DaCosta Sr., Mwenyekiti wa Bodi
Bi. Deirdre P. Pierce, Mwenyekiti Msaidizi
Bi. Anna Hill
Bi. Whitney McGinniss
Bi. Allyson Gevertz
Bi. Vickie B. Turner
Dkt. Joyce Morley

Dkt. Devon Q. Horton, Msimamizi

Tarehe 13 Oktoba 2023

Wapendwa Familia za Wilaya ya Shule ya Kaunti ya DeKalb,

Ninamwandikia leo wakati huu ambapo kumekuwapo na wasiwasi na hisia kali kutokana na matukio ya hivi karibuni yanayotokea eneo la Mashariki ya Kati. Tunapokabilia na athari za ukatili huu wa kutisha, natumai kufikia kila mtu katika jamii ya wilaya ya shule ili kutoa hakikisho na kusisitiza umuhimu wa umoja na uangalifu wakati wa nyakati hizi zenye changamoto.

Usalama na ustawi wa wanafunzi, wafanyakazi, familia na jamii yetu bado ni muhimu katika kila shule, kituo na mali ya Wilaya ya Shule ya Kaunti ya DeKalb (DCSD). Kutokana na hayo, nasisitiza kwamba, hadi sasa, hakujaripotiwa vitisho au vitendo vyovyote vya vurugu ndani ya shule zetu vinavyohusiana na matukio ya kutisha nje ya nchi.

Hata hivyo, tumechukua hatua za ziada za kiusalama. Maafisa wetu wa Polisi wa DCSD, idara za usalama wa chuo, wasimamizi wa shule, na wafanyakazi wameelekezwa wawe waangalifu hasa katika kutambua na kuchunguza vitisho au ugomvi wowote unaoweza kutokea kuhusiana na matukio haya.

Bado, hii lazima iwe juhudi ya pamoja. Hatuwezi kuwa salama tukiwa peke yetu, kwa hivyo tunawahimiza wanajamii wote, vijana kwa wazee, wahusike kikamilifu katika kampeni yetu ya “*Shuhudia Jambo, Sema Jambo*”. Iwapo wewe au mtoto wetu atashuhudia au kushuku hali yoyote isiyosalama ndani au karibu na shule zetu- hata katika ujirani wetu- tunawahimiza mtahadharishe wafanyakazi wetu mara moja. Ushiriki wako katika juhudi hizi ni muhimu kwa mkakati wetu wa kudumisha usalama wa jumla.

Tunaendelea kuamini kwamba njia wazi za mawasiliano ni muhimu kati ya shule na familia zetu. Iwapo una maswali au wasiwasi wowote au unahitaji taarifa zaidi, tafadhali usisite kuwasiliana na wasimamizi wa shule yako.

Katika nyakati hizi zisizo na uhakika, tunakuomba tushirikiane kwa umoja na tuazime kudumisha ulinzi na usalama wa wanafunzi, wafanyakazi, familia na wanajamii wetu kama kipaumbele chetu kikuu zaidi. Asante kwa usaidizi na uelewa wako. Kwa pamoja, tutahakikisha kwamba shule zetu zinasalia kuwa mahali salama pa kujifunza, ukuaji na maendeleo.

Wako wa Dhati,

Dkt. Devon Q. Horton, *Msimamizi*
Wilaya ya Shule ya Kaunti ya DeKalb